

MKATABA WA KUPANGISHA NYUMBA

(Nyumba / Chumba / Fremu ya biashara)

Mkataba huu umefanywa leo tarehe mwezi mwaka, kati ya:

MWENYE NYUMBA

Jina kamili:

Namba ya NIDA: Simu:

Anwani:

MPANGAJI

Jina kamili:

Namba ya NIDA: Simu:

Kazi / Biashara:

1. KINACHOPANGISHWA

Mwenye nyumba anampangisha mpangaji **nyumba / chumba / fremu ya biashara** (futa kisichohusika) namba kilichopo Mtaa, Kata, Wilaya, Mkoa

2. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utanza tarehe na kuisha tarehe (miezi). Unaweza kuongezwa kwa makubaliano ya maandishi ya pande zote mbili.

3. KODI

Kodi ni TZS kwa mwezi (kwa maneno:). Italipwa kila miezi, kabla ya au tarehe ya mwezi, kwa njia ya taslimu / M-Pesa / Mixx by Yas / Airtel Money / HaloPesa / benki (futa isiyohusika). Malipo ya awali: miezi, jumla TZS Kila malipo yatatolewa risiti.

4. AMANA (DHAMANA)

Mpangaji amelipa amana ya TZS Itarudishwa ndani ya siku baada ya mkataba kuisha na nyumba kukabidhiwa, baada ya kutoa gharama za uharibifu (kama upo) na madeni yaliyobaki.

5. HUDUMA

Umeme (LUKU): Maji: Taka:

Ulinzi:

(Andika nani analipa: mwenye nyumba au mpangaji.)

6. MASHARTI

Kuchelewa kulipa kodi kwa zaidi ya siku kutasababisha adhabu ya asilimia ya kodi ya mwezi huo.

Mpangaji hataruhusiwa kupangisha tena (sub-let) wala kukaribisha wakazi wengine wa kudumu bila idhini ya maandishi ya mwenye nyumba.

Uharibifu wowote wa makusudi au wa uzembe utakaosababishwa na mpangaji au wageni wake utagharamiwa na mpangaji.

Mpangaji hatafanya mabadiliko ya kimuundo (kuta, milango, umeme, mabomba) bila idhini ya maandishi.

Mwenye nyumba ana haki ya kukagua baada ya kutoa notisi ya saa 24, isipokuwa dharura.

Matengenezo makubwa (paa, kuta, mabomba makuu) ni jukumu la mwenye nyumba; madogo ya kila siku ni ya mpangaji.

Mpangaji atatunza usafi wa nyumba na maeneo ya pamoja, na atafuata sheria za mtaa na za nchi.

Kwa fremu ya biashara: biashara inayoruhusiwa ni; mpangaji atakuwa na leseni na vibali vyote vinavyohitajika.

7. KUVUNJA MKATABA

Upande wowote unaweza kuvunja mkataba kwa kutoa notisi ya maandishi ya siku Kodi iliyolipwa kabla kwa kipindi ambacho mpangaji hatakaa itarudishwa / haitarudishwa (futa isiyohusika).

8. MIGOGORO

Mgogoro wowote utasuluhishwa kwanza kwa mazungumzo. Ikishindikana, utapelekwa kwenye vyombo vinavyohusika, ikiwa ni pamoja na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

9. MASHARTI YA ZIADA

.....
.....

Mwenye nyumba — jina, sahihi, tarehe

Mpangaji — jina, sahihi, tarehe

Shahidi wa mwenye nyumba — jina, sahihi

Shahidi wa mpangaji — jina, sahihi

Kiolezo cha bure kutoka nyumbazangu.com · Tuma risiti na mikataba kwa simu: app ya Nyumba Zangu